

# **Nini unapaswa kujua kuhusu Programu za Umma**

**1. Wakimbizi na wenyeukimbizi wunaweza kupata msaada kutoka SSI, TANF, misaada ya chakula na faida kamili kutoka MaineCare.** Hii ina maana kwamba kama umeomba ukimbizi na unasubiria maamuzi, mara utakapo pata hadhi ya ukimbizi utakubalika kwenye program hizi.

**2. Bila kujali hali yako ya uhamiaji kama uko nchini Marekani kihalali unaweza kupata :**

- **Msaada wa Jumla** kutoka mji wako au mji;
- **SSI** itasaidia kulipa mahitaji ya msingi kama una umri wa zaidi miaka 65 au kama una ulemavu;
- Faida ya **MaineCare** kama ni mjamzito au chini ya miaka 21, na

**3. Katika baadhi ya familia, baadhi ya watu wanaweza kupata msaada kutoka kwa programu za umma wakati wengine hawawezi.** Kwa mfano, mama anaweza asiwe na hadhi ya kupata MaineCare lakini watoto wake wakastahili. Hii ina maana kwamba unahitaji kufikiria kama mtu yeyote katika familia yako anakubaliwa.

**4. Huna haja ya kuonyesha ushahidi wa hali yako ya uhamiaji kama unaomba msaada kwa ajili ya jamaa wa familia yako na sio wewe.**

- Kama unaomba kwa ajili ya familia , unapaswa kuwaambia/kumuambia mfanyakazi wa DHHS kwamba maombi hayahusiani na wewe.
- Kama umesema haya, na mfanyakazi wa kesi anauliza kuhusu ushahidi wa hali yako ya uhamiaji, unaweza kusema **HAPANA.**

**5. Sheria inasema kwamba kama mtoto anakubalika kupata msaada, mtoto anatakiwa asaidiwe hata kama hautojibu swali kuhusu hali yako ya uhamiaji.**

**6. Kama hauna nyaraka za ukaaji kihalali unaweza kupata msaada katika program zifuatazo:**

- Msaada wa Matibabu ya Dharura;
- WIC (chakula kwa ajili ya wanawake wajawazito na watoto);
- Chakula cha mchana shuleni.
- Kinga, upimaji na tiba ya dalili za magonjwa ya kuambukiza;
- Head Start; na

- Makazi kwa wasio na malazi na waathirika wa ukatili wa majumbani. .

**Kwa maswali wasiliana na:**

<b>Maine Equal Justice Partners</b>	<b>Immigrant Legal Advocacy Project (ILAP)</b>
207-626-7058 <b>au</b> piga bure katika 1-866-626-7059	207-780-1593 <b>au</b> piga bure katika 1-800-497-8505
<a href="http://www.mejp.org">www.mejp.org</a>	<a href="http://www.ilapmaine.org">www.ilapmaine.org</a>